

# TIRA Updates 2024

Kwa Soko Salama la Bima

Toleo No.01 | Jarida la Mtandaoni | [www.tira.go.tz](http://www.tira.go.tz)



**BIMA**  
**Ni Kinga,**  
Leo na Kesho!



# Je, Unafahamu Kuhusu Bima ya Afya kwa Wote ?

*Suala la afya ni la kila mmoja*

## 1. Bima ya Afya kwa Wote ni nini ?

Ni bima inayotolewa na Skimu ya Bima za Afya kwa ajili ya kuhakikisha kila mtanzania anapata huduma ya afya kwa kutumia bima kwenye vituo vya afya na hospitali bila kikwazo chochote cha kiuchumi au kifedha.

## 2. Bima ya Afya kwa Wote nikwa ajili ya nani ?

"Bima ya Afya kwa Wote" ni kwa ajili ya kila Mtanzania, bila kujali hali ya kipato, ajira, au makazi. Lengo kuu ni kuhakikisha kila mtu anapata huduma bora za afya\* kwa gharama nafuu. Hii inajumuisha wafanyakazi wa sekta rasmi na isiyo rasmi, wakulima, wafanyabiashara, wajasiriamali, pamoja na wale ambao hawana ajira ya kudumu. Ni mango unaolenga kuhakikisha kila mtanzania anapata bima ya afya ili kupunguza migo wa gharama za matibabu na kuboresha upatikanaji wa huduma za afya kwa wote.

## 3. Bima ya Afya kwa Wote ina Umuhimu gani?

Bima ya afya ni muhimu kwa ustawi wa afya ya familia yako na jamii kwa ujumla. Inakupata kupata matibabu na kuepuka gharama za ghafla za matibabu ukiwa na uhakika wa kupata huduma za afya mwaka mzima bila kulipia gharama kubwa.

## 4. Bima ya Afya kwa Wote Inafanyaje Kazi?

Skimu ya Bima ya Afya kwa Wote inatekelezwa kwa mujibu wa kanuni rasmi zinazosimamiwa na TIRA. Mchakato wa usajili unalenga kuwafikia raia wote, wakiwemo wasio na uwezo, kupitia mfuko maalum wa serikali ili kuhakikisha kila mmoja anapata huduma kwa bora unaostahili.

## 5. Hatua za Usaili na Jinsi ya Kujiunga na Bima ya Afya kwa Wote

Kujiunga na Bima ya Afya kwa Wote, hatua ni rahisi

1. Tembelea kituo cha usajili cha karibu,
2. Fuata miongozo ya skimu za bima,
3. Sajiliwa na anza kunufaika ndani ya siku 30.

## Jarida Hili limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma

**Mhariri**  
Hadija Maulid

**Waandishi**  
Tabia Mchakama  
Anna Massao

**Msanifu**  
Abubakari W. Kafumba

TIRAUpdates ni jarida la mtandaoni linaloandaliwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) kupitia kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma, likilenga kutoa taarifa muhimu, kuelimisha, na kuhamasisha umma kuhusu sekta ya bima nchini. Jarida hili limeandaliwa kwa ili kufikia wadau mbalimbali wa sekta, wakiwemo mawakala wa bima, kampuni za bima, watoa huduma na watumiaji wa bima.

Jarida la TIRAUpdates litakuwa na taarifa za matukio mbalimbali, ikijumuisha uzinduzi wa miradi mipya, semina na warsha za mafunzo, na mikutano muhimu inayofanyika ndani ya sekta ya bima. Kwa kupitia jarida hili, wadau wataweza kufuatilia kwa karibu sera na mabadiliko ya sheria yanayoathiri sekta ya bima, pamoja na hatua zinazochukuliwa na TIRA kuboresha utendaji wa sekta.

Mbali na taarifa za matukio, TIRAUpdates itakuwa na makala maalumu zinazolenga kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa bima. Makala hizi zitaelezea kwa undani namna bima inavyofanyika kazi, aina mbalimbali za huduma na bidhaa za bima, na jinsi huduma hizi zinavyoweza kusaidia watu binafsi, familia, na biashara kukabiliana na dharura au majanga.

Aidha, toleo hili litaangazia matukio, habari na taarifa muhimu zilizotokea katika mwaka 2024.

Kwa mawasiliano zaidi wasiliana nasi  
kwa barua pepe  
[info@tira.go.tz](mailto:info@tira.go.tz)  
Au  
Piga simu bure +255 222 132 537

Tovuti yetu  
[www.tira.go.tz](http://www.tira.go.tz)

SCAN KUSOMA KIDIITALI



# TAHARIRI

## TIRA Yapambania Afya ya Kila Mtanzania Kupitia Bima ya Afya kwa Wote

Katika harakati za kujenga taifa lenye afya bora na ustawi wa jamii, Bima ya Afya kwa Wote imeibuka kuwa moja ya vipaumbele vikuu vya serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA). Mpango huu wa kimkakati unalenga kuhakikisha kwamba kila Mtanzania, bila kujali hali yake ya kifedha au kijamii, anapata huduma bora za afya kwa gharama nafuu na kwa wakati muafaka.

Bima ya Afya kwa Wote haizungumzii tu huduma za matibabu kwa wachache wenye uwezo, bali ni haki ya kila raia. Hii ni dhamira ya kimaendeleo inayolenga kupunguza mzigo wa kifedha ambao umekuwa ukielemea familia nyingi zinapokutana na dharura za kiafya. Kwa mara ya kwanza, Watanzania watapata urahisi na uhakika, wakijua kwamba afya zao ziko mikononi mwa mfumo wa kitaifa unaosimamiwa na TIRA, mfumo unaohakikisha usawa na ufanisi wa huduma za afya.

Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote inawalenga zaidi wale wasio na uwezo, ambapo serikali imeweka mfuko maalum wa kuwahudumia. Kwa hatua hii, TIRA inadhihirisha kwa vitendo kuwa hakuna Mtanzania anayepaswa kukosa huduma za matibabu kwa sababu ya ukosefu wa fedha.

Huu ni mwamko mpya unaolenga kuvuka mipaka ya changamoto za kiafya na kuhakikisha kuwa hakuna anayeachwa nyuma. Kupitia ushirikiano na wadau mbalimbali, serikali imefanikiwa kuanzisha miradi ya mfano kama ule wa bima kwa Watanzania 10,000, ambao umeleta matumaini mapya kwa wengi. Huu ni uthibitisho kwamba Bima ya Afya kwa Wote ni zaidi ya wazo, bali ni ukweli unaotimia hatua kwa hatua.

Tunapoangazia mustakabali wa taifa letu, suala la afya limekuwa ni msingi wa maendeleo endelevu. Taifa lenye afya ni taifa linaloweza kushindana katika ngazi za kimataifa kiuchumi na kijamii. Kwa kupitia mpango huu, TIRA inaendelea kujenga msingi thabiti wa afya kwa kila Mtanzania, bila kujali hali zao za maisha.

Kwa pamoja, tunalo jukumu la kuhamasisha kila mmoja ajiunge na Bima ya Afya kwa Wote ili kuhakikisha afya na ustawi wa taifa letu vinapewa kipaumbele cha juu. Sasa ni wakati wa kufanya maamuzi sahihi kwa afya yetu, afya ya familia zetu, na afya ya taifa kwa ujumla.

Kwa pamoja tujenge Ustawi wa afya kwa Wote!

**Dkt. Baghayo A. Saqware**  
Kamishna wa Bima Tanzania  
TIRA



- 1 Palipo na Huduma ya Benki, Bima Inapatikana
- 3 Baraza la Maulid Kitaifa: TIRA Yakabidhi Ofisi ya Waziri Mkuu Bima za Afya 1,093 kwa Wenye Mahitaji Maalumu
- 4 Wanawake na Bima: Zoezi la Bima Elfu Moja Lawafikia JUWAKITA
- 6 Siku ya Bima Yafana: Wadau Sekta ya Bima Wafanya Mkutano Mkuu Dodoma
- 7 Waziri Prof. Mkenda Asifu Kazi ya TIRA, Ataka Waendeleo Kuvutia Wawekezaji Wazawa
- 8 TIRA Yafanya Ukaguzi wa Bima za Vyombo vya Moto, Zaidi ya Magari 200 Yakaguliwa Manyara
- 9 TIRA na Jamii, Jamii na Tira: TIRA Yatoa Zawadi Fainali Polisi Jamii Cup
- 10 Bima ni Kinga na Uwekezaji - Dkt. Baghayo: Maadhimisho Wiki ya Bima 2024
- 11 Uzinduzi wa Umoja wa Mawakala Wa Bima Wanawake, Wajipanga Kuleta Mageuzi Sekta Ya Bima
- 13 Waendesha Pikipiki Wapewa Elimu Ya Bima na Kufundishwa Jinsi Ya Kutumia Mifumo ya TIRA Kuhakiki Bima Zao
- 14 Kamishna wa Bima Tanzania Asikiliza Maoni na Kutoa Ufafanuzi wa Masuala ya Bima
- 15 Maadhimisho ya Bima Yafana Zanzibar
- 16 Endesha Salama, Ufike Salama, Bima ni Kinga Yako
- 17 Elimu Kuhusu Bima Yatolewa kwa Kamati za Kudumu za Bunge za PIC za PAC
- 19 TIRA Yatoa Misaada Hospitali ya Somanda na Shule ya Sekondari Bariadi
- 20 Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi la TIRA Wafanyika Mkoani Lindi
- 22 TIRA Yashiriki Mkutano wa Wanawake kwenye Sekta ya Fedha
- 24 TIRA Yakutana na Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu SMZ
- 25 TIRA Yafanya Mkutano na Wadau wa Usafrishaji
- 26 Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi Aipongeza Sekta ya Bima
- 27 Ukuaji Soko na Bima Umechangiwa na Uwekezaji Bora na Soko la Bima Imara
- 29 TIRA Yachangia Zaidi ya Milioni 20 Kuboresha Hospitali ya Rufaa ya Amana
- 30 Dkt. Saqware Asisitiza Umuhimu wa Bima ya Afya Kwa Wote
- 32 Igunga Waitika Wito wa Serikali Kukata Bima ya Zao la Mpunga

01



02





# Palipo na Huduma ya Benki, Bima Inapatikana:

PBZ Sasa Rasmi Wakala Wa Bima



Naibu Kamishna wa Bima, Bi. Khadija Said alizindua rasmi huduma ya benki wakala wa bima ya Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ Bancaassurance) tarehe 23 Julai 2024 Zanzibar.

Hafla hiyo fupi iliwaleta pamoja wadau wa sekta ya bima wakiwemo kampuni za bima ambazo zitashirikiana na PBZ kutoa huduma za bima kupitia benki.

Benki ya PBZ imepiga hatua kubwa ya kimaendeleo kwani sasa huduma za bima zitakuwa zinapatikana kwenye matawi yote ya PBZ yaliyopo mijini na vijijini kauli mbiu ikiwa "Palipo na huduma ya benki, Bima inapatikana".

Huduma ya Benki wakala wa Bima nchini imeendelea kukua kwa kasi hadi kufikia asilimia 15 kwa mwaka 2024. Hii inaonyesha jinsi

gani huduma hii imepokelewa vema na wananchi.

"Hali hii inaleta matumaini makubwa kwamba tuko kwenye njia sahihi ya kuhakikisha kuwa kila Mtanzania anapata huduma bora za bima kupitia benki wakala", amesema Naibu Kamishna wa Bima, Bi. Khadija Said.

Aidha, amewataka Benki wakala wa bima wote

kufuata miongozi iliyowekwa katika kutoa huduma za benkibima ili soko la bima likibakia kuwa endelevu.

Naibu Kamishna pia alizipongeza kampuni za bima ambazo tayari zimeshajiunga na PBZ lakini pia aliwasisitiza wale ambao bado hawajajiunga na PBZ wafanye hivyo ili kuongeza ushindani zaidi katika kutoa huduma Bora za Bima kwa watazania.







# Baraza la Maulid Kitaifa:

## TIRA Yakabidhi Ofisi ya Waziri Mkuu Bima za Afya 1,093 kwa Wenye Mahitaji Maalumu

Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) imekabidhi kadi za bima za afya 1,093 kwa Waziri Mkuu Mhe. Kassimu Majaliwa wakati wa Baraza la Maulid lililofanyika Septemba 16, 2024 mkoani Geita.

Awali kabla ya kukabidhi kadi hizo Kamishina wa Bima Tanzania Dkt. Baghayo Saqware alisema Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan alisaini Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote (UHI) namba 13 ya mwaka 2023 ili kuwezesha watanzania wote kunufaika na bima.

Katika kukamilisha azma hiyo, Mufti na Sheikh Mkuu wa Tanzania Dkt. Abubakar Zuber bin Ally na Kamishna wa Bima Tanzania, Dkt. Baghayo Saqware walianzisha zoezi la kutoa bima za afya 10,000 kwa watanzania mbalimbali bila kujali tofauti zao.

Awamu ya kwanza ya utoaji bima hizo elfu kumi, Dkt. Saqware amekabidhi kadi za bima 1,093 ambapo kadi 500 ni za kampuni ya Assemble na zilizobaki 593 ni za Kampuni ya Strategis. Mchakato wa kadi zilizosalia 8,907 utaendelea kutekelezwa kwa awamu chini ya kamati maalum ya Mufti ili kufikia ahadi ya

kadi elfu kumi.

Bima hizo zimekidhi vigezo vyote vya kisheria na kati

ya bima hizo wanaume watapata kadi 448 na wanawake kadi 605. Aidha, kadi hizo zimeshalipiwa



hivyo, wanufaika wataweza kupata huduma za afya na matibabu mwaka mzima bila kugharamia chochote kwenye Hospital zote nchini ambazo zina mkataba na Kampuni au Skimu ya bima ya afya.

Wazo hili la kuwafikia watanzania wenye uhitaji

wa bima za afya lilikuja wakati wa uzinduzi wa kitabu cha Mufti chenye maudhuhi ya maadili.

Zoezi hili kwa upande wa pili litawaunganisha watanzania wengi bila kubagua wala kujali dini, kabila, jinsia ama umri kwa kua suala la afya ni la wote.



# Wanawake na Bima:

## Zoezi la Bima Elfu Moja Lawafikia JUWAKITA



Jumuiya ya Wanawake wa Kiislamu Tanzania (JUWAKITA) wamepatiwa elimu ya bima kupitia shughuli maalum iliyoandaliwa na wanawake hao katika Mkoa wa Geita wakiongozwa na viongozi wao wakiwemo Mwenyekiti wa JUWAKITA Taifa, Mama Shamim Khan na Mwenyekiti Jumuiya hiyo Mkoa wa Geita, Mama Zaituni Hussein pamoja na wajumbe wengine.

Elimu hiyo ilitolewa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) ikiwakilishwa kwenye tukio hilo na Bw. Ayubu Mremi, Afisa Takwimu Bima na Bw. Abubakari Kafumba, Afisa

Uhusiano kwa Umma ambapo lengo kuu lilikua ni kuwafikishia elimu ya bima akina mama hao ili wapate uelewa wa masuala ya bima na umuhimu wake ili kupata uhakika wa matibabu pindi magonjwa yanapoibuka pasipo kutarajiwa.

Zoezi hii ni likikua ni muendelezo wa utekelezaji wa ahadi ya Kamishna wa Bima Tanzania, Dkt. Baghayo Saqware na Mufti na Sheikh Mkuu wa Tanzania, Sheikh Dkt. Abubakar Zuber ya kutoa bima za afya kwa watanzania ambapo katika awamu ya kwanza zilitolewa bima elfu moja

bure.

Jumuiya hiyo inawakilisha kundi kubwa la akina mama walio na wasio waislamu kwenye jamii zetu wakiwa ndio walezi wakuu kwenye ngazi ya familia. Katika misingi ya malezi bora miongoni mwa jamii zetu, ni dhahiri kuwa mama akiwa kama mlezi wa familia ndio anayesimamia kuhakikisha si tu familia zinapata malezi bora bali pia wanachangia kuhakikisha kaya zinakuwa na ustawi wa afya njema hasa kujikinga na maradhi na kupata matibabu inapotokea mmoja ameugua.

Hivyo, elimu hiyo ya bima waliyopata wanawake hao itaendelea kuwajenga kuwa mabalozi bora sio tu kwenye ngazi ya familia lakini pia kuwahamasisha makundi mengine katika jamii kutumia fursa kama hii kuhakikisha wanakua mstari wa mbele katika kukuza jamii zenye muamko wa kujikinga na kukabiliana na madhara ya majanga au changamoto zisizotarajiwa za kiafya pindi inapohitajika kupata matibabu.

Mwenyekiti wa JUWAKITA, Mama Shamim Khan aliwasisitiza akina mama hao kuchangamkia fursa



hio kwa kujiandikisha ili kupata bima hizo za afya kwa ustawi wa afya ya familia zao na jamii kwa ujumla.

Kwa kuwa mama ndio mlezi mkuu ni rahisi kuchangia katika kufanya maamuzi sahihi ili kulinda afya za wanafamilia wanapohitaji kupata matibabu. Alisema, "Tayari bima imefika milangoni kwenu, wote tumeona faida ya bima, msilaze damu wala msikate tamaa. Ombi langu kwenu akina mama nendeni

mkajiandikishe kwakuwa bima hizi zinazotolewa ni bure, changamkieni fursa hii".

Katika kuhakikisha elimu hiyo ya bima inawafikia vena akina mama hao, Bw. Ayubu Mremi alisema, "Ni dhahiri kuwa wanawake kuwa akina mama kunawapa sehemu kubwa katika malezi kwenye jamii zetu. Bima hizi elfu moja zilizotolewa ni bure kabisa, hivyo wewe na familia yako mtaweza kupata huduma za matibabu bila kuingia gharama yoyote kwa

mwaka mzima. Hii itasaidia kuondoa changamoto ya kukosa matibabu kutokana na ukosefu wa fedha".

Kupitia zoezi hili la utoaji elimu ya bima elfu moja, ni wazi kuwa TIRA imepiga hatua kubwa katika kuhakikisha akina mama, kama nguzo muhimu za familia, wanapata uelewa juu ya umuhimu wa bima ya afya. Elimu waliyoipata itawawezesha kuwa mabalozi wa mabadiliko ndani ya familia zao na jamii kwa ujumla. Wito wa viongozi wa JUWAKITA

unasisitiza kuwa akina mama wachangamkie fursa hii ya bima bure ili kuhakikisha ustawi wa afya za familia zao.

TIRA inaendelea kuthibitisha dhamira yake ya kuwafikia wananchi wote na kuwajengea uwezo wa kukabiliana na changamoto za kiafya kupitia huduma za bima. Hili ni jambo la kupongezwa na linatoa mwamko na hamasa ya kuweka afya mbele kwa kila familia.



# Siku ya Bima Yafana:

## Wadau Sekta ya Bima Wafanya Mkutano

### Mkuu Dodoma

Mkutano wa kila mwaka wa Siku ya Bima ulifanyika Septemba 14, 2024 jijini Dodoma ambapo wadau mbalimbali katika sekta ya bima wamekutana Mgeni Rasmi akiwa ni Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Makundi Maalum Mhe. Dorothy Gwajima (MP).

Mkutano huo ulikua ni mwendelezo wa Wiki ya Bima 2024 na uliandaliwa na Taasisi ya Bima (IIT) kwa kushirikiana na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) ukiwa na lengo la kukutanisha wadau wa bima wakiwemo kampuni za bima, vyuo/taasisi za bima na watumiaji wa huduma za bima ili kujadili mambo mbalimbali kuhusu sekta ya bima nchini.

Katika hotuba yake Mhe. Gwajima aliipongeza TIRA kwa majukumu yake katika kutoa elimu ya bima Tanzania na kusisitiza elimu ya bima kutolewa zaidi kwa jamii. "Kaeni na vyuo vya Maendeleo ya Jamii wapewe elimu (wanachuo) ili kuongeza sauti ya sekta ya bima".

Mhe. Gwajima pia alisisitiza Kauli mbiu hii ya mwaka huu "Bima jumuiishi: bidhaa zinazokidhi mahitaji na usambazaji wa Kiteknolojia" ikatufanye tuwe na tafakuri ya mpango mkuu wa maendeleo ya sekta ya fedha 2020 – 2030 kwa sekta ndogo ya bima, sambamba na



maelekezo ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.





# Waziri Prof. Mkenda Asifu Kazi ya TIRA, Ataka Waendelelee Kuvutia Wawekezaji Wazawa



Mgeni Rasmi kwenye uzinduzi wa maonesho ya wiki ya huduma za fedha Tanzania Mhe. Prof. Adolf Mkenda ambae ni Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia alisifu shughuli zinazofanywa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima ya kusimamia sekta hiyo muhimu kwa taifa huku akiitaka taasisi hiyo kuendelea kuweka miundombinu itakayovotia wawekezaji wengi zaidi wa sekta ya bima kutoka Tanzania.

Ameyasema hayo wakati alipotembelea Banda la TIRA kwa ajili ya kujionea shughuli mbalimbali zinazofanywa na Mamlaka hiyo. Waziri Mkenda

alisema, sekta ya bima mbali ya kusaidia kuingia majanga mbalimbali yanayotokea lakini pia ni sekta ambayo watanania wanapaswa kutumia fursa iliyopo ili kuweza kuwekeza kwa kufungua kampuni ili kuweza kujiingizia kipato binafsi na taifa kwa ujumla.

Akijibu swali kuhusu njia zinazofanywa na Mamlaka ili kuvutia uwekezaji kwa wazawa, Mwanasheria Jamal Mwasha ambae ni Msajili wa Migogoro ya Bima katika Ofisi ya Msuluhishi wa Migogoro ya Bima amesema Sheria ya Bima sura ya 394 kupitia kifungu cha 16 imeweka sharti kuwa kila kampuni inayoanzishwa nchini,

lazima walau theluthi moja imilikiwe na wazawa.

Kwahiyo Mamlaka ina hakikisha kifungu hiki kinazingatiwa ipasavyo na sharti hilo linatimizwa, amesema pia Mamlaka inatumia majukwaa mbalimbali inapokutana na wawekezaji na wadau wa sekta nyingine kuwapa elimu juu ya fursa zilizopo na kumekua na mwikio mzuri.

Mwasha alimalizia kusema kuwa Mamlaka inasaidia uanzishwaji wa Konsotia ya Bima ya Kilimo ambapo ni muunganiko wa kampuni wazawa walioweka mtaji ili kuweka ufanisi katika utekelezaji wa Skimu ya

Taifa ya Bima ya Kilimo na kuongeza uwezo wa kimtaji wa soko la bima nchini kwa ajili ya kuingia majanga kwenye sekta ya kilimo.

Awali alipomkaribisha Mhe. Waziri kwenye Banda la TIRA, Meneja Uhusiano na Mawasiliano Bi. Hadija Maulid ameeleza kuwa TIRA inashiriki kwenye Maonesho ya wiki ya huduma za kifedha pamoja na wadau wa kampuni za bima kwa lengo la kutoa elimu kwa umma wa Tanzania kuhusu umuhimu bima lakini kwa kampuni zinazoshiriki zinatoa huduma za moja kwa wananchi wanaohitaji kukata bima mbalimbali.

# TIRA Yafanya Ukaguzi wa Bima za Vyombo vya Moto, Zaidi ya Magari 200 Yakaguliwa Manyara

Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) kupitia ofisi yake ya Kanda ya kati iliyopo jijini Dodoma, imefanya ukaguzi wa vyombo vya moto katika eneo la Mererani wilayani Simanjiro mkoani Manyara.

Ukaguzi huo ulianza Septemba 9 na kumalizika Septemba 12, 2024 ambapo magari zaidi ya mia mbili (200) yamekaguliwa huku zoezi hilo likilenga kukagua bima katika vyombo hivyo vya moto na kutoa elimu ya umuhimu wa kutumia bidhaa za bima.

Ukaguzi huu wa vyombo

vya moto unafanywa kwa kushirikiana na wadau wengine kama Jeshi la Polisi, Kikosi cha Usalama barabarani, EWURA, kampuni za bima na wakala wa bima.

Pia vituo mbalimbali vya mafuta vilifanyiwa ukaguzi ili kuhakikisha sheria na kanuni za bima zinafuatwa. Na hii ni kutokana na sheria ya Mafuta ya mwaka 2015 ambayo inavitaka vituo vyote vya mafuta kuwa na bima ya majanga.

Faida ya Bima ya vyombo vya moto ni pamoja na kumsaidia mtumiaji kujikinga na hasara pindi anapopata ajali na pia

usalama pale anaposababisha ajali kwa mtu mwingine.

TIRA Kanda ya Kati inahudumu mikoa ya Dodoma, Manyara na Singida.





# TIRA na Jamii, Jamii na Tira:

## TIRA Yatoa Zawadi Fainali Polisi Jamii Cup



Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) Septemba 7, 2024 ilijumuika pamoja na wananchi mbalimbali wa Ikwiriri wilayani Rufiji kuhitimisha mashindano ya Polisi Jamii Cup ngazi ya Mkoa wa Kipolisi Rufiji.

TIRA ilidhamini mashindano hayo ambayo yaliwakutanisha wadau mbalimbali wakiwemo polisi na kampuni za Bima. Kurudisha kwa Jamii (ufadhili) hasa katika michezo, ni jambo ambalo Mamlaka ya Usimamizi wa

Bima imekuwa ikifanya kwa lengo la kuileta jamii karibu na kutoa elimu kuhusu bima.

Afisa Bima Ndg. Joseph Mfoi alihitimisha kwa kutoa elimu ya bima kwa wananchi waliokusanyika katika uwanja wa Mabatini lengo likiwa kila Mwananchi afahamu na kutumia Bidhaa za bima.

Pia Mratibu Mkuu wa Polisi Jamii Mkoa wa Kipolisi Rufiji, ASP J. B Ibrahim aliishukuru Mamlaka kwa kuendeleza ushirikano

Mara kwa mara. Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania ina jukumu la kutoa elimu ya bima, kulinda na kuendeleza soko la bima nchini,

kusimamia kampuni za bima na hata kuishauri Serikali kuhusu masuala la bima nchini. Lengo ni kuhakikisha kila Mtanzania anafahamu kuhusu bima.





# “Bima ni Kinga na Uwekezaji” - Dkt. Baghayo:

Maadhimisho Wiki ya Bima 2024



Wiki ya Bima kwa mwaka 2024 ilifanyika rasmi Septemba 13, 2024 jijini Dodoma ambapo Kilele cha Wiki ya Bima nchini kiliadhimishwa Septemba 14, 2024 ambapo wadai mbalimbali wa Bima walikusanyika kwa pamoja na kufanya matembezi ya kilometa tano kutoa elimu ya bima nchini na matumizi ya huduma za bima.

Wiki ya Bima iliandaliwa na Taasisi ya Bima Tanzania (IIT) kwa ushirikiano na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA).

Lengo lilikuwa ni kuwaleta pamoja wadai wa bima na kujadili mambo mbalimbali kuhusu sekta hiyo muhimu hapa nchini. Na hufanyika kila mwaka.

‘Utaratibu huu (maadhimisho) unasaidia wananchi kuamini sekta ya bima na kutumia huduma mbalimbali za bima ambazo zitawasaidia kuondokana na umaskini.

Bima ina dhumuni la kutoa kinga na pia ni uwekezaji hivyo tunawashauri watazania wote watumie bima” alisema Dkt.

Baghayo Saqware, Kamishna wa Bima Tanzania.

Aidha, Mhe. Janet Mayanja Mkuu wa Wilaya ya Chamwino akimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Dodoma aliipongeza sekta ya bima nchini na kusisitiza elimu ya bima iendelee kutolewa kwa wananchi ili wazitumie kwa faida yao.



# Uzinduzi wa Umoja wa Mawakala Wa Bima Wanawake, Wajipanga Kuleta Mageuzi Sekta Ya Bima



Wanawake kutoka Umoja wa Mawakala wa Bima Wanawake Tanzania (UMABIWATA) wamejipanga kuleta mageuzi kwenye Sekta ya Bima nchini kwa kuhakikisha kuwa wanafanya kazi kufuata misingi na taratibu zote za kibima. Hayo

yamebainishwa wakati wa Uzinduzi wa Umoja wa Mawakala wa Bima Wanawake Tanzania (UMABIWATA) uliofanyika tarehe 5 Septemba 2024 jijini Arusha.

Katika uzinduzi huo Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Mhe. Felician Mtahengerwa

alikuwa mgeni rasmi huku viongozi na wadau kutoka Kampuni mbalimbali za bima na Sekta wakishuhudia.

Mhe. Felician alieleza kuwa umoja huu unaakisi maendeleo na mafanikio ya jitihada zinazofanywa na Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kupitia Mamlaka husika inayosisamia Sekta ya Bima nchini TIRA.

Kwa kuwa dharura na majanga hayatokei kwa taarifa, ni vema jamii ziendelee kuelimishwa na kuhamasishwa umuhimu





wa kuchukua tahadhari kwa kutumia huduma mbalimbali za bima.

Akiwakilisha Mamlaka ya Usimami wa Bima, Meneja wa Kanda ya Kaskazini, Bw. Bahati Ogolla amesema kuanzishwa kwa UMABIWATA ni hatua muhimu katika kuhakikisha kwamba wanawake wanapata nafasi sawa na fursa ya kuingia na kufanikiwa katika sekta ya Bima.

Chama hiki kimedhamiria kuongeza tija na wigo katika utoaji huduma kwenye soko la Bima

Tanzania, ili kuwezesha wanawake wengi zaidi kuwekeza kwa kua mawakala wa Bima.

Aidha, ameendelea kusema kuwa kupitia programu mbalimbali wanawake wataweza kusaidiana kitaalamu katika maswala yanayohusu Bima ili hatimaye kusaidiana wakati wa shida kama vile kufiwa, ugonjwa ama kuunguliwa na moto.

Pia, wataweza kukua kiuchumi, kuboresha hali za kijamii kwa kutoa ajira mbalimbali, kutoa elimu ya bima, kuongeza wigo wa

kuwafikia Watanzania, pamoja na kuchangia ukuaji wa soko la Bima.

Katiba wa UMABIWATA, Bi. Edina Mgage alisema kuwa chama hicho kitaendelea kushirikiana na kampuni mbalimbali za bima, wadau mbalimbali na Mamlaka inayosimamia Sekta.

Bi. Mgage amesema, "Lengo letu hapo baadae ni kufungua kampuni ya Bima ya Wanawake ambayo itakua ya kwanza Tanzania na Africa tukifuata mfano wa benki ya wanawake tanzania (Tanzania Women's Bank).

Ndoto yetu kama wanawake wenye uthubutu ni kuendelea kuwa mstari wa mbele kuziinua jamii zetu ili ndoto zetu zisipeperuke au kubaki kuwa nadharia tu bali tuwe chama chenye kuacha alama 'legacy' katika soko letu la bima nchini".

Mafanikio makubwa ya Sekta ya Bima hayataweza kupatikana pasipo ushirikiano imara na ushirikishwaji wa wadau wengine muhimu wa sekta ndogo ya bima.



# Waendesha Pikipiki Wapewa Elimu Ya Bima na Kufundishwa Jinsi Ya Kutumia Mifumo ya TIRA Kuhakiki Bima Zao



Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) imeendelea na utoaji wa elimu ya bima kwa jamii katika makundi mbalimbali ili kuhakikisha wanawafikia watanzania wengi zaidi ili wajue na watambue huduma za bima. Tarehe 31 Agosti 2024,

katika viwanja vya Tip top jijini Dar es Salaam, Mamlaka kupitia ofisi yake ya Kanda ya Mashariki inayodumu mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, na Pwani kwa kushirikiana na wadau wa bima, ilitoa elimu ya bima katika Bonanza la Bodaboda

ambapo waendesha bodaboda walipata fursa ya kufahamu mfumo wa kuhakiki chombo cha moto kupitia TIRA-MIS.

Aidha waendesha bodaboda hao walielezwa umuhimu wa kukata bima na gharama za bima kwa

usafiri wa bodaboda, zaidi ya hapo, walipata fursa ya kuuliza maswali yaliyopatiwa majibu papo hapo. Ujumbe wa TIRA uliongozwa na Afisa Bima Ndg Mfoi pamoja na Haiba, Abdul, Islam, John na Kalebi Chiya.

# Kamishna wa Bima Tanzania Asikiliza Maoni na Kutoa Ufafanuzi wa Masuala ya Bima



Kamishna wa Bima Tanzania, Dr. Baghayo Saqware alikutana na wadau wa kampuni za bima tarehe 31 Agosti 2024 katika ofisi za Mamlaka visiwani humo kujadiliana mambo mbalimbali yanayohusu bima.

Wawakilishi wa kampuni hizo za bima walitoa maoni na changamoto zao mbalimbali ambazo zilisikilizwa na kutolewa ufafanuzi na Kamishna wa Bima Tanzania pamoja na Naibu Kamishna wa Bima

Tanzania Bi. Khadija Said. Kikao hicho pia kilihudhuriwa na mameneja wa TIRA Zanzibar kwa upande wa ofisi ya Unguja na Pemba.

Dkt. Saqware alizitaka kampuni hizo za bima kuendelea kuweka mikakati mbalimbali katika utoaji wa elimu ya bima ili kila mtanzania aweze kufahamu umuhimu wa bima na kunufaika na huduma hiyo, pia moja ya changamoto iliyotajwa na wadau hao ni udanganyifu

katika bima ambapo Kamishna wa Bima Tanzania amesema,

“Udanganyifu katika bima ni jambo ninalotamani kuona limeisha, tunaendelea kulifanyia kazi na ikiwa kuna mashaka yoyote juu ya udanganyifu ni vizuri mtutaarifu mapema”.

Pia Naibu Kamishna wa Bima Tanzania alisisitiza kampuni hizo za bima kuendeleza ushirikiano wa pamoja na ziendele

kujikita zaidi katika kutoa elimu kwa umma.

Kikao hicho kimeenda sambamba na kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Bima Zanzibar yaliyofanyika katika uwanja wa Mao Zedong Agosti 31, 2024, mgeni Rasmi akiwa ni Mhandisi Zena Said Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi Zanzibar.



# Maadhimisho ya Bima Yafana Zanzibar: “Serikali Haiwezi Kufumbia Macho Magari Kukosa Bima” – Mhe. Zena Said



Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania kwa kushirikiana na wadau wa bima wamefanya maadhimisho ya Siku ya Bima yaliyojumuisha matembezi ya hiari katika kukuza uelewa wa elimu ya bima visiwani humo tarehe 31 Agosti 2024.

Matembezi hayo yalianzia katika uwanja wa Mnara wa Kisonge, Michenzani mpaka uwanja wa Mao

Zedong ambapo maadhimisho hayo yamefanyika.

Mgeni Rasmi katika Maadhimisho hayo alikua Mhe. Mhandisi Zena Said, Katibu Mkuu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi Zanzibar.

Mhe. Zena Said amesema “Serikali haiwezi kufumbia macho magari kukosa bima, tutafanya kazi na

taasisi zingine wasiingie ili wasiweze kuingia barabarani, pia nawaasa viongozi wa serikali kukatia bima mali zao”

Tukio hilo pia lilihudhuriwa na Kamishna wa Bima Tanzania Dkt. Baghayo Saqware na Naibu Kamishna wa Bima Tanzania Bi. Khadija Said, pamoja na Makatibu Wakuu, Manaibu Katibu Wakuu na wadau

mbalimbali katika sekta ya bima.

Matembezi ya Bima Zanzibar ni tukio la kila mwaka linaloandaliwa ili kuongeza uelewa kuhusu umuhimu Zanzibar.

Tukio hili limekuwa likifanyika kwa ushirikiano wa wadau wa sekta ya Bima.

# Endesha Salama, Ufike Salama, Bima ni Kinga Yako



yafunguliwe rasmi ni chachu kwa madereva, waendesha pikipiki na watumiaji wote wa barabara. Kila mmoja anapaswa kwa namana moja au anyingine aguswe na suala la Usalama Barabarani. Ajali nyingi zinazotokea ni kwa sababu ya mapungufu ya kibanadamu.

Serikali imeendelea kuchukua hatua ili kupunguza ajali zinazoweza kuzuilika kama vile ujezi wa barabara, matumizi ya mifumo ya kudhibiti mwendo wa magari na kudhibiti magari mabovu kuingia barabarani. Haya yote yanakwenda sawia na kila mmoja kuchukua tahadhari na hatua kuisalama”.

Mhe. Kihenzile alivetoa rai kwa wadau na waahiriki wote wa Usalama Barabarani kuzingatia mkakati uliotolewa na Baraza la Usalama Barabarani. Wapanda pikipiki kuacha kuendesha pikipiki bila kupata mafunzo, bila kua na leseni barabarani, kuacha tabia ya kubeba abiria zaidi ya mmoja na kutoendesha bila kuvaa kofia ngumu. Watumiaji wengine wa barabara sote tuzingatie sheria za barabarani.

Kwa wanaotumia magari kuacha tabia ya kushabikia mwendonkasi na kutokubali kusongamana kwenye magari.

Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) imepokea tuzo ya hongera kwa kushiriki kwenye Maonesho ya Maadhimisho ya Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani, yaliyofanyika kuanzia tarehe 26 Agosti hadi tarehe 01 Septemba 2024 katika viwanja vya Jamhuri jijini Dodoma.

Katika hafla maalum ya kufunga rasmi maadhimisho hayo Naibu Waziri wa Uchukuzi na Kaimu Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Usalama

Barabarani Mhe. David Kihenzile alikua mgeni rasmi na alikabidhi tuzo na vyeti kwa washiriki mbalimbali waliofanya vizuri ikiwemo Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tani w.

Mamlaka ya Usimamizi wa Bima (TIRA) ilipata fursa ya kupaza sauti kwa kutoa elimu ya bima na jinsi Sekta ya Bima inavyochangia katika kupunguza na kukabili madhara yanayotokana na ajali za barabarani kwa kutumia huduma ya Bima ya Vyombo vya Moto.

Kupitia kaulimbiu ya mwaka huu “Endesha Salama, Ufike Salama” Mamlaka imewafikia wataanzania hususani wakazi wa Dodoma na mikoa mingine ya jirani kwa kuwakumbusha wataanzania kuwa Usalama Barabarani ni la kwetu sote na kila mmoja akichukua hatua kiekuka ajali na kujikinga na madhara ya ajali inawezekana.

Mhe. Kihenzile alisema, “Elimu ambayo imekua ikitolewa tangu maadhimisho haya



# Elimu Kuhusu Bima Yatolewa kwa Kamati za Kudumu za Bunge za PIC za PAC



Mwenyekiti wa Bodi ya Taifa ya Bima CPA Moremi Marwa pamoja na Wenyevitwa Kamati za Bodi hiyo Dkt. Suleiman Mohamed Na Bw. Justine Mwandu wameungana na Menejimenti ya TIRA kutoa elimu kuhusu maswala mbalimbali ya bima kwa Kamati za Kudumu za bunge za Uwekezaji Mitaji

kwa Umma (PIC) na Hesabu za Serikali Mwezi Mei 30, 2024 Bungeni jijini Dodoma.

Elimu hiyo ilyotolewa kwa viongozi hao ililenga kuwapa uelewa ili nao waweze kuwa mabalozi wazuri kwa wananchi wao pindi wanapokutana kwenye shughuli mbalimbali kwenye

majimbo yao.

Watoa huduma mbalimbali za bima wakiwemo Kampuni za bima, bima mtawanyo na benki wakala wa bima nao walishiriki kutoa uelewa kuhusu huduma mbalimbali zinazotolewa kwenye kampuni zao.

Awali Ujumbe kutoka TIRA na Wadau wake watoa huduma za bima walihudhuria Kikao cha Bunge cha bajeti cha Wizara ya Ujenzi kwa mwaliko wa Mhe. Japhet Hasunga (Mb) na Mhe. Wanu Hafidh (Mb) ambao wote ni Mabalozi wa Bima.







# TIRA Yatoa Misaada Hospitali ya Somanda na Shule ya Sekondari Bariadi



Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) kupitia Kanda ya Ziwa na kwa kushirikiana na kampuni za bima tarehe 23 Agosti, 2024 walitoa misaada mbalimbali katika Hospitali ya Somanda na shule ya Sekondari ya Bariadi, wilayani Bariadi, Simiyu.

Vifaa mbalimbali kwa ajili ya matumizi ya binadamu vilitolewa kama sabuni,

taulo za kike, mipira, daftari Aidha, Mkurugenzi wa wilaya ya Bariadi Ndg. Adrian Jungu alikuwepo katika tukio hilo, akimuwakilisha Mkuu wa Mkoa huo Mhe. Kenan Kihongosi.

Baada ya utolewaji wa misaada hiyo, baadhi ya washiriki walipata nafasi ya kufanya kikao mkakati kuimarisha soko la Bima nchini.





# Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi la TIRA Wafanyika Mkoani Lindi



Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) ilifanya Mkutano wake wa Sita wa Baraza la Tatu la Wafanyakazi Mkoani Lindi Februari 15, 2024 kwa lengo la kujadili, kutafakari na kutoa ufumbuzi kwa changamoto na mambo mbalimbali yanayowakabili Watumishi na Sekta ya Bima ya Jumla.

Awali akisoma Risala yake Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi ambao pia ni Kamishna wa Bima Tanzania Dkt. Baghayo Saqware alisema Sekta ya bima imeendelea kukua mwaka hadi mwaka na hii ni kutokana na juhudi za pamoja zinazofanywa na Watumishi wa TIRA na Wadau mbalimbali. "

Sekta imekua kwa wastani wa asilimia 26.7 kwa mwaka 2022.

Ni wazi kuwa ongezeko hili linatokana na juhudi mbalimbali za Wajumbe wa Baraza ambazo mmekuwa mkizichukua kwa kushirikiana na wananchi, Mamlaka, Wizara ya Fedha na Serikali kwa Ujumla" Amesema Dkt. Saqware.

Akaongeze kuwa Juhudi hizo ni pamoja na kuweka mazingira wezeshi ya kuvutia wawekezaji kuja kuwekeza kwenye Sekta ya bima, kuongeza usimamizi na kuendeleza soko kwa kuandaa miongozo mbalimbali ya bima na kubuni mifumo ya tehamu au kidigitali kwa ajili ya usimamizi na pia utoaji wa elimu kwa umma kupitia



vyombo mbalimbali vya habari.

Kwa upande wake Mgeni Rasmi wa Mkutano huo Dkt. Mohamed Suleiman, ambae ni Makamu Mkt. wa Bodi ya Taifa ya Bima aliwataka Watumishi kuendeleza uadilifu na kujituma ili kufikia malengo ya Serikali ya kukuza uwekezaji nchini ambapo Sekta ya Bima ina fursa kubwa ya kukatia bima miradi hiyo ya uwekezaji.

Alisema ni Jukumu la Watumishi wa Mamlaka ambao Serikali imewakasimu majukumu nyeti ya kuishauri katika masuala mbalimbali kwenye sekta ya Bima kuwa wabunifu na kufikiria zaidi juu ya huduma na bidhaa ambazo zinaendana na majanga yaliyopo na kutatua changamoto za kiuchumi na za kijamii zinazowakabili wananchi wetu na shughuli zao.

Nae Katibu wa Baraza Bw. Richard Toyota alisema Mkutano huo wa Sita wa Baraza la Tatu, unafanyika kwa Siku Mbili na utajadili kwa uwazi maswala ya bajeti lakini pia hoja mbalimbali zilizowasilishwa na Watumishi kwa Ufafanuzi.

Alisema kauli mbiu ya Uwazi na Ushirikishwaji inaendana na uhalisia wa namna TIRA inaendesha shughuli zake.





# TIRA Yashiriki Mkutano wa Wanawake kwenye Sekta ya Fedha



Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) kwa kushirikiana na Chama cha Wanawake Waliopo Kwenye Sekta ya Fedha (TAWIFA) pamoja na Taasisi ya Mwanamke foundation (MIF) waliadhimisha Siku ya Mwanamke duniani kwenye sekta ya fedha iliyofanyika tarehe 14 Machi, 2024 katika Ukumbi wa Kwanza Hotel uliopo

Kizimkazi Mkoa wa Kusini Unga.

Maadhimisho hayo yaliambatana na Uzinduzi wa Chama cha Wanawake Waliopo kwenye Sekta ya Fedha ambapo Mgeni Rasmi wa shereke hizo alikuwa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Wakati wa hotuba yake ya uzinduzi wa TAWIFA Dkt. Samia amewataka wanawake wajibiidishe katika kazi zao ili waweze kupata nafasi za juu katika kukuza uchumi wa nchi kupitia sekta ya fedha. Aliendelea kwa kusema kuwa wanawake sasa tutoke kwenye harakati tuje kwenye utendaji au utekelezaji wa harakati hizo

ili tusonge mbele katika maendeleo ya jamii na nchi kwa ujumla.

Sherehe hizo zilihudhuriwa na wanawake wengi wakiwemo viongozi kama vile Mawaziri, Wake wa Marais waliopita, wakuu wa Taasisi pamoja na viongozi wa chama na serikali.







# TIRA Yakutana na Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu SMZ



Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) ilifanya Mkutano na Makatibu Wakuu pamoja na Manaibu Katibu Wakuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) tarehe 22 Machi 2024 ambapo Mgeni Rasmi alikua ni Mhandisi Zena Ahmed Said Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi SMZ

Kikao hicho kilichowakutanisha pia Watendaji Wakuu wa NIC, ZIC, EARE, PDB na Msajili wa Hazina kilipokea matokeo ya tathmini

iliyofanywa na TIRA kuhusu ukatiwaji wa Bima wa Mali za Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Akifanya Wasilisho lake Kamishna wa Bima Dkt. Baghayo Saqware amesema, Kwa upande wa Bima za Vyombo vya Moto na Bima za Afya, SMZ imefanya vizuri kwa zaidi ya asilimia 80 na kuwaomba watendaji hao wakuu wa Serikali kuendelea kutilia mkazo kwenye upande wa bima nyingine kwani zinasaidia kuinga mali za serikali

dhidi ya Majanga mbalimbali.

Kwa upande wake Katibu Mkuu Kiongozi ambaye pia ni Balozi wa Bima amewataka Makatibu hao kufanya tathmini ya mali zote zilizopo kwenye Wizara zao na pia kufanya tathmini ya gharama za malipo ya bima ili kusaidia kufanya maamuzi yenye tija. Ameongeza kuwa ni vyema pia watendaji hao kupatiwa uelewa mpana juu ya aina mbalimbali za bima.

Awali akitoa neno la Ukaribisho Naibu Kamishna wa Bima Tanzania Bi. Khadija Said amesema, Mamlaka imejidhatiti kutoa ushirikiano ili kurahisisha huduma za bima Visiwani Zanzibar na kwamba hivi karibuni TIRA itafungua ofisi nyingine Pemba na ofisi nyingine Unguja.

Kikao hicho ni mfululizo wa utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka yanayolenga kukuza soko la bima nchini.



# TIRA Yafanya Mkutano na Wadau wa Usafirishaji



Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania TIRA kupitia Kanda ya Mashariki ilifanya Mkutano na Wadau wa maswala ya usafirishaji wenye lengo la kutoa elimu na kupata uelewa wa pamoja kuhusu bima.

Mkutano huo uliofanyika Aprili 25, 2024 jijini Dar es Salaam uliwakutanisha Viongozi wa Wamiliki wa

Mabasi, viongozi wa chama cha waendesha Bodaboda na Bajaji, viongozi kutoka Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, Viongozi chama cha kutetea abiria, mwakilishi kutoka LATRA na ATI.

Mada mbalimbali kuhusu mfumo wa uhakiki wa bima, bima kwa mabasi ya abiria, sheria ya bima kwa

vyombo vya moto na usalama barabarani, sheria na kanuni za usafirishaji na majumkumu ya vyama vya usafirishaji.

Akiongea wakati wa majumuisho ya majadiliano ya mkutano huo Ndugu Zakaria Muyengi ambae ni Meneja wa TIRA Kanda ya Mashariki amesema, Mkutano huo umefungua

ya kuwa na mikutano ya aina hiyo Kanda ya Mashariki na kwamba wadau hao na wengine watahusishwa mara kwa mara. Muyengi alitoa rai kwa viongozi hao kuwasiliana na Mamlaka ama kufika ofisi za Mamlaka zilizopo jengo la PSSSF Samnujoma.



# Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi Aipongeze Sekta ya Bima



Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi Mhandisi Zena Ahmed Said aliipongeza Sekta ya Bima kwa juhudi inazochukua kwa ajili ya kutoa Elimu kwa Umma wa Watanzania lakini pia kwa kutoa huduma za bima ambazo ni rafiki kwa kila Mtanzania.

Aliyasema hayo Julai 3, 2024 alipotembelea Kijiji cha Bima kwenye Maonesho ya 48 ya Kimataifa ya Biashara maarufu Sabasaba ambapo kampuni za bima 40 zinashiriki kwa kutoa elimu na huduma mbalimbali za

kibima. Mhandisi Zena ambae pia ni Mwenyekiti wa Mabalizi wa Bima Nchini amesema ni vyema Kampuni hizi kwa kushirikiana na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) kuendelea kutumia majukwaa mbalimbali kutoa elimu kwakuwa Wananchi wengi hawana bima hivyo wakipata uelewa watajikinga na majanga kupitia bima kwani sekta imetengeneza bidhaa za bima ambazo ni rafiki kwa Wananchi ikizingatiwa pia bima nyingine zinalipiwa kidogokidogo kwa kila mwezi hivyo wananchi

wengi wanaweza kumudu. "Nimeona kuna bima zinazochangiwa mpaka Tzs 2,000/= kwa mwezi, toeni elimu kwa lugha nyepesi wananchi wakielewa watakata bima kwani zina manufaa" alisisitiza Mhandisi Zena.

Kwa upande wake, Meneja wa Kanda ya Mashariki TIRA Bw. Zakaria Muyengi alimshukuru Mhandisi Zena kwa kuwa mstari wa mbele kuhakikisha bima

inaeleweka ipasavyo kwa wananchi na viongozi serikalini kwa kutilia mkazo wa mara kwa mara juu ya umuhimu wa Bima.

Wadau wa Sekta ya Bima bado wanaendelea kutoa huduma mbalimbali Katika Kijiji cha Bima kilichojizolea umaarufu kwa unadhifu na mpangilio mzuri wa huduma.

Karibu 77, karibi Kijiji cha Bima.



# Ukuaji Soko na Bima Umechangiwa na Uwekezaji Bora na Soko la Bima Imara

– Naibu Waziri Fedha



Mgeni Rasmi katika Uzinduzi wa Taarifa ya Utendaji wa Soko la Bima kwa mwaka 2023 Mhe. Hamad H. Chande; Naibu Waziri wa Fedha wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameeleza kufurahishwa na ukuaji wa soko la bima hapa nchini.

“Nimeshuhudia ongezeko la wasajiliwa utoaji huduma za bima ukiongezeka kutoka watu elfu moja mia moja na sitini na tano (1165) kwa mwaka 2022 hadi watu elfu moja mia nne na sabini na mbili (1472) kwa mwaka 2023, hili limechangiwa na uwekezaji mzuri na soko la

bima imara” amesema.

Mhe. Chande pia ameeleza ripoti hiyo inatoa hali halisi, picha ya wazi na taswira ya soko la bima nchini na kuipongeza Bodi ya Taifa ya Bima, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima (TIRA) pamoja na kamati ya maandalizi kwa uandaaji

wa Taarifa hiyo muhimu ikizingatiwa pia TIRA ni miongoni mwa sekta za fedha zinazochangia kuongeza pato ya Serikali.

Naibu Waziri pia aliipongeza Mamlaka kwa kujenga mahusiano ya karibu na mazingira wezeshi kwa watoa





huduma za bima na kusisitiza uendeleu wa mafanikio hayo kwasababu Serikali chini ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imeweka mazingira bora ya uwekezaji.

Lakini pia alitoa angalizo kwa Mamlaka kufatilia

uwepo wa bima katika sekta ya michezo ambapo vijana wengi watafikiwa katika huduma za bima, lakini pia Mamlaka kuendelea kuongeza kasi ya matumizi ya kidigitali ili kurahisisha utolewaji wa huduma za bima.

Zaidi pia alizitaka kampuni za bima kufanya kazi kwa uaminifu kwasababu Serikali imeziamini kwa kutoa leseni ili waweze kufikisha huduma bora kwa wataanzania na kusisitiza uwekezaji zaidi katika sekta za mafuta na gesi, usafiri, utalii, kilimo, mifugo, uvuvi

na nyinginezo na mwisho alitoa neno kuhusu bima ya afya kwa wote;

“Bima ya Afya kwa Wote ni mkakati utakaoleta mageuzi makubwa katika sekta ya afya kwa wataanzania”



# TIRA Yachangia Zaidi ya Milioni 20 Kuboresha Hospitali ya Rufaa ya Amana



Mamlaka ya Usimamizi wa Bima (TIRA) ilishiriki kwenye halfa ya Harambee iliyopewa jina la 'Rafiki wa Amana Dinner Gala 2024' iliyofanyika jijini Dar es Salaam iliyoandaliwa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam kwa kushirikiana na Hospitali ya Rufaa ya Amana ambapo mgeni rasmi alikuwa Mhe. George Simbachawene, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejiment ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Akihudhuria hafla hiyo, Kamishna wa Bima Tanzania, Dkt. Baghayo

Saqware alisema kuwa TIRA imechangia zaidi ya milioni 20 kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa majengo ya watoto njiti, wajawazito pamoja na kununua vifaa tiba ili kuboresha Hospitali ya Rufaa ya Amana ikiwa ni moja ya hatua za kushiriki kijamii katika kuhakikisha watanzania wanapata huduma za afya za uhakika.

Dkt. Saqware ameongeza kuwa nia ya Mamlaka ni kuona huduma za afya zinazotolewa ni zenye ubora na zenye uhakika. Hatua hii ya kuchangia kwenye kwenye sekta ya afya pia kutaiendeleza

Sekta ya Bima kwakua watumiaji wa huduma za afya pia ni watumiaji wa bima. Matarajio ni kwamba kupitia Bima ya Afya kwa Wote (UHI) na uboreshaji wa hospitali kama Amana, wananchi wengi zaidi wataweza kupata huduma za afya kwa urahisi na kwa gharama nafuu.

Aidha, jitihada hizi zinachochea lengo la serikali la kuhakikisha kila Mtanzania anapata huduma za afya kupitia mfumo wa bima, ambao unatoa fursa kwa wananchi kulipa gharama za matibabu kwa usalama na

kuondoa mzigo wa gharama zisizotarajiwa.

TIRA inaamini kuwa afya bora inachangia katika maendeleo ya jamii, na hivyo, Mamlaka inajitolea kuendelea kushirikiana na sekta ya afya katika kampeni na miradi inayolenga kuboresha ustawi wa wananchi. "Lengo letu ni kuona kila Mtanzania anapata huduma bora za afya na kwamba hakuna mtu anayeachwa nyuma kutokana na kukosa uwezo wa kugharamia matibabu," alisema Dkt. Saqware.

# Dkt. Saqware Asisitiza Umuhimu wa Bima ya Afya Kwa Wote:

Ziara ya Kutoa Elimu ya Bima kwa Mkoa wa Njombe



Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) kupitia Ofisi ya Kamishna wa Bima na ujumbe wake walitembelea Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Njombe ikiwa ni muendelezo wa ziara ya kuwatembelea Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya katika Kanda ya Juu kusini inayojumuisha Mikoa ya Songwe, Mbeya, Njombe, Ruvuma, Mtwara na Lindi.

Ujumbe huo ukiongozwa na Kamishna wa Bima, Dkt. Baghayo Saqware ulikutana na watumishi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Njombe wakiongozwa na Kaimu Katibu Tawala Njombe, Bw. Edward Mwakipesile

ambapo lengo kuu la ziara hii ni kutoa elimu ya bima kwa wakuu wa mikoa na wilaya ili waweze kuhimiza matumizi ya bidhaa na huduma za bima katika jamii zao na hatimaye kuweka misingi ya ushirikiano na taasisi mbalimbali kwa ajili ya kulinda haki za watumiaji wa bima na kuhakikisha huduma za bima zinawafikia wananchi kwa urahisi na uwazi.

Aidha, Dkt. Saqware alieleza kuhusu umuhimu na hatua za utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ili kuwahimiza wananchi

hususan wananjombe na hatimaye wawe watumiaji wa bima hiyo.

Kwa mujibu wa takwimu, sekta ndogo ya Bima imeendelea vizuri kila mwaka ambapo watoa huduma za Bima wanaongezeka kwa zaidi ya asilimia 10% hadi kufikia watoa huduma 1,610 mwaka 2023.

Aidha, watumiaji wa bidhaa na huduma za Bima wameongezeka kutoka milioni 6 mwaka 2022 hadi kufikia milioni 12 mwaka 2023 sawa na asilimia 20 ya wananchi, amesema Dkt. Saqware.

Kwa muktadha huu Kamishna wa Bima pia alisema kuwa ili kufikia ukuaji wa Sekta ndogo ya bima kwa angalau asilimia 15 katika miaka 5 ijayo, Mamlaka imeainisha vipaumbele kadhaa ikiwemo ukamilishaji wa Sera ya Bima ya Taifa na mkakati wake wa utekelezaji, ukamilishaji wa Kanuni za Bima ya Afya kwa Wote na Miongozo husika ya usimamizi, ukamilishaji wa Kanuni za Bima za Lazima, ukamilishaji wa Kanuni za Bima za Kilimo, uanzishaji na utekelezaji wa Skimu ya Taifa ya Bima za Kilimo, ukamilishaji wa utaratibu wa kisheria wa





uanzishwaji wa Bodi ya Wataalam wa tasnia ya Bima, Hifadhi ya Jamii na Utathminishaji (ISPAB).

Kupitia tukio hili Mamlaka iliomba Ofisi ya Mkuu wa Mkoa iwahamasisha wakuu wa wilaya, Makatibu tawala na wananchi wa mkoa wa Njombe kutekeleza Sheria ya Bima ya Afya kwa wote na kutoa ushirikiano katika kuhakikisha elimu ya bima

inawafikia wananjombe na kujenga uelewa wa bima ili wabaini manufaa ya kutumia bima kama kinga mahsusi kwa maisha, afya na mali zao.

wa upekee mkubwa Kamisha wa Bima, Dkt. Baghayo Saqware alitumia fursa hiyo pia kumuomba Mkuu wa Mkoa wa Njombe Mhe. Anthony Mtaka kuwa Balozi wa TIRA katika utoaji

wa elimu ya bima kwa wananjombe, kuwahamasisha kutumia bidhaa na huduma za bima, hususan bima za afya na kilimo.

Sambamba na hilo, Kamishna alimtabulisha Meneja wa Kanda ya Juu Kusini Bi. Neema Lituli ambaye atahakikisha Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Njombe inapatiwa ushauri wowote

wa kitaalamu kuhusu bima akishirikiana na Kampuni za bima zilizopo kwenye Kanda ya Juu Kusini.

Kupitia ofisi za kanda, Mamlaka itaendelea kuhakikisha soko la bima la Tanzania linaendela kuwa himilivu, lisilo na udanganyifu, lenye weledi na lenye tija.



# Igunga Waitika Wito wa Serikali Kukata Bima ya Zao la Mpunga



Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania kupitia ofisi ya Kanda ya Magharibi, Tabora ikiwakilishwa na Meneja wa Kanda hiyo Dkt. Emmanuel Lupilya imetoa elimu ya bima na kuwahamasisha wakulima wa Kijiji Cha Mwampuli, Wilaya Igunga mkoani Tabora katika tukio muhimu ambapo Mkuu wa Mkoa wa Tabora Mhe. Paul Matiko Chacha alikua mgeni rasmi.

Wakulima hao wa zao la Mpunga wamepewa elimu ya bima na kuhamasishwa umuhimu wa kukata bima

ya zao hilo kwa kufuatia melekezo ya Serikali yanayomtaka kila mkulima kuwa na bima ya kilimo kwa ajili ya kuwasaidia waweze kusonga mbele zaidi na sio kurudi nyuma pindi wanapopatwa na majanga yasiyotarajiwa.

Mhe. Chacha amesisitiza kwamba Bima ni huduma isiyopingika na ni maelekezo ya Serikali kuwa kila mkulima lazima awe na Bima ya kilimo.

Hivyo, ni vema wakulima wakatamia fursa hiyo kuitikia wito huu ili

kuhakikisha wanashiriki kwenye kilimo kwa tija.

Dkt. Lupilya akiwakilisha Mamlaka amesema kuwa kwa sera iliyopo inaelekeza kila mkulima anapaswa kuwa na bima kwa ajili ya maghala ya mpunga, mashine za kilimo cha mpunga mpaka kiwandani, Bima ya Shambani ili kujikinga na majanga yasiyotarajiwa, yanayopelekea kupunguza wastani wa makisio ya mavuno, ubora wa zao la mpunga, lakini kubwa ni kutumia Bima hiyo kwa ajili ya Mkopo kwenye taasisi za

fedha.

Aidha, kupitia uhamasishaji uliofanywa na Mamlaka wakulima, viongozi wa bodi, mameneja, katibu meneja, wajumbe wa bodi na viongozi wa AMCOS zaidi ya 500 wameitikia wito wa Serikali kwa kuonyesha utayari wa kuchukua tahadhari ya kujikinga na majanga yasiyotarajiwa kuanzia msimu huu wa kilimo 2024/2025 kwa kukatia bima mazao na maghala yao.





# TIRA & 2024

**Mamlaka ya Usimamizi wa Bima**  
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania  
PSSSF HOUSE, 5th Floor, Makole Street, P.O. Box 2987  
DODOMA, Tanzania.

coi@tira.go.tz  
+255 26 2321180  
+255 0222135137  
+255 26 2321180

**FB, IG, X: //@tira\_tz**  
[www.tira.go.tz](http://www.tira.go.tz)